


# MY BICYCLE

# BAISIKELI

# YANGU



swahiliKIDS

# JE, WEWE UNAJUA?

Tarehe Tatu mwezi wa Sita ni  
siku ya baiskeli Duniani!

Je, wewe una **baiskeli**?  
Je, unapenda **baiskeli**?



Did you know?  
June third is World Bicycle Day!  
Do you have a bicycle?  
Do you like bicycles?

**Mimi nina baiskeli nzuri.  
Baiskeli ya rangi ya waridi.**



**I have a nice bicycle.  
A pink bicycle.**

Baiskeli yangu ina matairi  
mawili meusi.



My bike has two black wheels.

**Mdogo wangu anajifunza  
kuendesha baiskeli ya matairi  
matatu.**



**My little brother is learning  
how to ride a tricycle.**

Baiskeli yangu ina kikapu cha  
rangi ya njano.



My bike has a yellow basket.

**Mimi napenda kuendesha  
baiskeli yangu hasa wakati  
wa kiangazi.**



**I like riding my bike especially in  
the summertime.**

**Mimi napenda kuendesha  
baiskeli yangu kwenda  
shule.**



**I like riding my bike to school.**

**Leo naendesha baiskeli  
kwenda uwanja wa michezo.**



**Today I am riding a bike to the  
playground.**

**Mimi naendesha baskeli  
yangu kila jioni kufanya  
mazoezi.**



**I ride my bike every evening to  
exercise.**

**Sisi tunavaa kofia kujikinga  
wakati tunaendesha baiskeli**




**We wear helmets to protect  
ourselves when riding a bike.**

**Mimi na rafiki yangu tunapenda  
kuendesha baiskeli zetu. Leo  
tunaendesha baiskeli zetu  
kwenda ufukweni.**



**My friend and I like riding our  
bicycles. Today we are riding our  
bikes to the beach.**

**Mimi na dada yangu tunapenda  
kuendesha baiskeli zetu. Sisi  
tunaendesha baiskeli zetu  
kwenda maktaba.**



**My sister and I love riding our  
bikes. We are riding our bicycles  
going to the library.**

**Mimi na familia yangu tunapenda kuendesha baiskeli kutunza mazingira. Sisi tunaendesha baiskeli kwenda kila mahali!**



**My family and I love riding bicycles to protect the environment. We are riding our bicycles to go everywhere!**

**Na wewe je?  
Unapenda kuendesha baiskeli?  
Unapenda kuendesha baiskeli  
yako kwenda wapi?**



**What about you?  
Do you like riding a bike?  
Where do you like to ride your  
bike to?**

# ZOEZI

Chagua jibu Sahihi- Pick the correct answer

1. Siku ya baiskeli duniani ni mwezi wa ngapi?

- a. Mwezi wa kwanza
- b. Mwezi wa sita
- c. Mwezi wa kumi


2. Tairi la baiskeli lina umbo gani?

- a. Duara
- b. Pembe tatu
- c. Mstatili

3. Tukiendesha baisikeli tunasaidia

- a. Kuchafua mazingira
- b. Kusoma vitabu
- c. Kutunza mazingira

# Watoto Mini Book Series by.....



# swahiliKIDS



<https://www.swahilikids.com>



@kiswahiliKIDS



@swahiliKIDS



@swahili.KIDS